



برے خاتے کے اسباب

Sababu Za Mwisho Mbaya

(Swahili)

Shaikh-e-Taariqat Ameer-e-AhleSunnat
Mwanzilishi wa Dawat-e-Islami,
Allama Moullana Abu Bilal

MUHAMMAD ILYAS
Attar Qadiri Razavi رحمۃ اللہ علیہ

مکتبۃ الدینیہ
Dawat-e-Islami

بُرے خَاتَمے کے اَسْبَاب

Sababu Za Mwisho Mbaya

Kijitabu hiki kiliandikwa na Shaykh-e-Tariqat Amīr-e-Aḥl-e-Sunnat, muanzilishi wa Dawat-e-Islami ‘Allāmah Maulānā Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qadiri Razavi دامت برکاتہم العالیة katika lugha ya Kiurdu. Kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Majlise Tarajim. Endapo utaona makosa yoyote katika tafsiri yake au utungaji wake, tafadhali wajulishe Majlise Tarajim kwa njia ya posta au kwa kipepesi ili upate thawabu.

Majlise Tarajim (Dawat-e-Islami)

Alami Madani Markaz, Faizan-e-Madina, Mahalla Saudagran,
Old Sabzi Mandi, Baab-ul-Madina, Karachi, Pakistan
Wasiliana kwa nambari: +92-21-34921389 hadi 91
translation@dawateislami.net

MAKTABA-TUL-MADINA

UK: 80-82 Bordesley Green Road, Birmingham, B9 4TA.

Contact: 07989996380 - 07867860092

E-mail: uk@dawateislami.net

USA: Faizan-e-Madina, P. O. Box 36216, Houston, Tx 77274.

Contact: +713-459-1581, 832-618-5101

INDIA: 19/20 Muhammad Ali Road, opposite Mandvi post office

Mumbai – 400 003.

Contact: +91-022-23454429

BANGLADESH: K.M Bhovan, 1st Floor, 11, Andar Killa Chittagong.

HONG KONG: Faizan-e-Madina, M/F-75, Ho Pui Street, Tsuen Wan N.T.

Contact: +85-98750884 – 31451557

SOUTH AFRICA: 61A, Mint Road, Fordsburg, Johannesburg.

Contact: 011-838 9099

KENYA: Kanz-ul-Iman, Near Al-Farooq Hospital, Tonoka Area Mvita, Mombasa.

Contact: +254-721-521916

TORONTO CANADA: 1060 Britannia Road Unit 20, 21 Mississauga ONT Canada.

Contact: +141-664-82261

MOZAMBIQUE: Mesquita Faizan-e-Madina Rua Alfredo Lawley, Esturro, Beira.

Contact: 00258-848554888 - 00258-822808580

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Du'a Kabla Ya Kusoma Kitabu

Kabla ya kusoma kitabu au somo la kidini, soma dua ifuatayo.

إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ utakumbuka yote uliyoyasoma.

اللَّهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَانْشُرْ
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

Tafsiri

Ee mola عَزَّوَجَلَّ ifungue milango ya elimu na busara kwa ajili yetu, na utuhurumie! Ewe ulie Mtakatifu kabisa.

(Al-Mustatraf Juzuu I, uk. 40, Dar-ul-Fikr, Beirut)

Kumbuka: Mswalie Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ mara moja kabla na baada ya dua.

Chati ya unukuu

ء	A/a	ژ	Ř/ř	ل	L/l
ا	A/a	ز	Z/z	م	M/m
ب	B/b	ژ	X/x	ن	N/n
پ	P/p	س	S/s	و	V/v, W/w
ت	T/t	ش	Sh/sh		
ٹ	Ṭ/ṭ	ص	Ṣ/ṣ	ة / ه / و	Ĥ/ĥ
ث	Š/š	ض	Ḍ/ḍ	ی	Y/y
ج	J/j	ط	Ṭ/ṭ	ے	Y/y
چ	Ch	ظ	Ẓ/ẓ	ِ	A/a
ح	H/h	ع	‘	ُ	U/u
خ	Kh/kh	غ	Gh/gh	ِ	I/i
د	D/d	ف	F/f	وِمدّه	Ū/ū
ڈ	Ḍ/ḍ	ق	Q/q	یِمدّه	Ī/ī
ذ	Ž/ž	ک	K/k	اِمدّه	Ā/ā
ر	R/r	گ	G/g		

Orodha Ya Yaliyomo

Du'a Kabla Ya Kusoma Kitabu	iii
Chati ya unukuu	iv

SABABU ZA MWISHO MBAYA..... 1

Madhara ya kutomswalia Mtume ﷺ	1
Hakuna anayeweza kutiwa katika ukafiri na ndoto	2
Hairuhusiwi kuandika ^ص badala Ya ﷺ	2
Pata manufaa ya mapumziko	3
Sababu nne za mwisho mbaya	3
Kisa cha ukorofi wa makosa matatu	5
Kufufuliwa kwa sura ya mbwa.....	6
Maana 'yakufitinisha watu'	6
Je, tunajiepusha na kufitinisha watu?.....	7
Maana ya wivu	9
Maelezo mepesi ya wivu	9
Kisa cha Qutb-e-Madinah	10
Kuangamia kwa muadhini wawili waliokuwa wakipenda amrad (wavulana wazuri wanaovutia).....	10
Hukumu ya stara	11
Kumuangalia amrad kwa matamanio ni haramu	12

Sababu za Mwisho Mbaya

Amrad ana mashetani sabini	12
Kutohiji ni sababu ya mwisho mbaya.....	13
Hofu ya mwisho mbaya kwa anayezungumza wakati wa adhan	13
Aliyeufuutiliza adhana aingia peponi.....	14
Mlima wa moto.....	15
Adhabu ya udanganyifu katika mizani.....	15
Mwisho mbaya wa shehe.....	16
Mwalimu wa zamani wa malaika	16
Shetani katika sura ya wazazi.....	16
Tone la maumivu ya kifo.....	17
Shetani kwa sura za marafiki.....	18
Tutakuwaje?	18
Udhibiti ulimi wako	18
Maua ya madani kwa mwisho mwema.....	19
Maombi manne ya kifo chenye imani	20
Masanduku ya moto.....	21
Kulia kwa mtume mtukufu ﷺ	22

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Sababu Za Mwisho Mbaya

Bila shaka shetani hatakuruhusu kusoma kitabu hiki. Ili kuelewa vitmbi vya shetani, kisome kitabu hiki kuanzia mwanzo hadi mwisho.



Madhara ya kutomswalia Mtume ﷺ

Inasemekana kwamba mtu mmoja alimuota mtu aliyekufa amevaa kofia ya majusi (wanaoabudu moto). Akamuuliza sababu ya kufanya hivyo. Akamjibu, “Nilikuwa simswalii Mtume mtukufu aliyebarikiwa صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kila niliposikia likitajwa jina lake. Dhambi hii imesababisha kupotea kwa imani yangu.”

(Sab'a Sanābil, uk. 35, Maktaba Nūrāh Razavīyyah, Sakhar)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Hakuna anayeweza kutiwa katika ukafiri na ndoto

Ndugu wapenzi waislamu! Mumeona madhara ya dhambi! Mtu anaweza kupoteza imani anapokata roho. Yafaa hapa tuzingatie hukumu hii: Ingawa ndoto mbaya kuhusu mtu ni jambo la kututia hofu lakini ndoto ya asiyekuwa mtume si ushahidi wa kisheria na muislamu hawezi kutiwa katika ukafiri kutokana na ndoto tu. Hata kama aliyekufa atamtokezea mtu katika ndoto akiwa na ishara ya kufuru au maiti mwenyewe amjulisha anayeota kuhusu kupotea kwa imani yake, hawezi kuitwa kafiri.

Hairuhusiwi kuandika ^صbadala ya ﷺ

Şadr-ush-Sharīʿah, Badr-uṭ-Ṭarīqah, ‘Allāmah Mufti Muhammad Amjad ‘Ali A’zamī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوِي amesema, “Ni faradhi (kwa muislamu) kumsalia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ mara moja katika uhai wake. Ni Wājib katika mkusanyiko wa waumini kumsalia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kila unapotaja au kulisikia jina lake likitajwa.

Hata kama mtu atalisikia jina la Mtume aliyebarikiwa صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ mara mia moja katika kikao kimoja amswalie kila anapotajwa. Ikiwa mtu atataja au kusikia jina lilobarikiwa na asimswalie wakati huo, basi amswalie wakati mwengine wowote. Kwa mujibu wa wanachuoni wengine, mtu anapoandika jina la Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ni wajib kuandika ‘صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ’. Watu wengi siku hizi hufupisha Şalāt-‘Alan-Nabī kwa kuandika ع, ص, عم, صلعم au (SAW) au (PBUH). Hili

haliruhusiwi na ni Haramu kali mno. Vile vile watu wengine huandika **بِض** au **بِ** badala ya **رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ** na **ح** badala ya **رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ**. Jambo hili yafaa tuliepuke.” (*Baḥār-e-Sharī‘at*, juzuu 3, uk.101-102, *Maktaba-tul-Madīnah, Karachi*). Baada ya kuandika jina tukufu la Allah **عَزَّوَجَلَّ**, tusiandike **ح** bali tuandike **عَزَّوَجَلَّ** au **جَلَّ جَلَالُهُ**.

Pata manufaa ya mapumziko

Ndugu waislamu wapenzi! Kisa kilichotangulia kimeeleza kuhusu mazingatio ya ndoto ya mtu aliyekufa ambaye hakumswalia Mtume **صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** alipotaja au kusikia jina lake. Tuogope kutojali mipango iliyofichika ya Allah **عَزَّوَجَلَّ**. Tusiwe wavivu kumswalia Mtume **صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ**.

Yawezekana mtu hapo zamani alipolitaja au kusikia jina la Mtume **صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** awe hakumswalia. Ikiwa ni hivyo, mtu amswalie sasa kwa kuwa sheria imemruhusu mtu kumswalia baadaye ikiwa wakati ule hakumswalia. Siku zijazo mtu ajaribu kumswalia Mtume **صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** punde tu anapotaja au kusikia akitajwa. Vinginevyo amswalie baadaye.

Sababu nne za mwisho mbaya

Imeandikwa katika Sharḥ-us-Şudūr kwamba kuna sababu nne za mwisho mbaya.

1. Uvivu katika kusimamisha swala
2. Kutumia vileo

3. Kutowatii wazazi
4. Kusababisha madhara kwa waislamu (*Sharḥ-us-Ṣudūr, uk. 27, Dār-ul-Kutub-ul-‘Ilmiyyah, Beirut*)

Ni jambo la kuzingatia kwa ndugu waislamu ambao hawasimamishi swala au hukidhi au hawaamki kuswali swala ya asubuhi au huswali nyumbani bila ya kuruhusiwa na sheria badala ya kuswali msikitini kwa jamaa. Uvivu katika kusimamisha swala usije ukasababisha mwisho mbaya! Vile vile yule ambaye anakunywa pombe, hawatii wazazi wake na husababisha madhara kwa waislamu aidha kwa ulimi au mikono yake, basi atubu kikweli kweli.

Maulānā Sayyid Muhammad Na’imuddīn Murādābādī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْهَادِي amesema, “Hakika, kutubu ni kurudi kwa Allah عَزَّوَجَلَّ.” Kuna nguzo tatu za kutubu:

1. Kukubali kuwa ulitenda dhambi.
2. Kujuta.
3. Kuazimia kuacha dhambi.

Ikiwa dhambi ya lipika, ni lazima uilipe. Kwa mfano ikiwa mtu amekosa swala, lazima aombe msamaha na aikidhi.” (*Khazāin-ul-‘Irfān, uk.12, Bombay*) Ikiwa mtu amewanyima wengine haki zao lazima awatimizie haki zao baada ya kutubu. Kwa mfano, ikiwa mtu amewaudhi wazazi wake, ndugu, mke, rafiki, au mtu yeyote, basi lazima aombe msamaha kwa njia ambayo atasamehewa. Haitoshi kusema ‘pole’ tu kwa kila jambo.

Kisa cha ukorofi wa makosa matatu

Imeandikwa katika Minhāj-ul-‘Ābidīn kwamba Sayyidunā Fuḍayl bin ‘Iyād رضي الله تعالى عنه siku moja alimtembelea mmoja wa wanafunzi wake ambaye alikuwa anakaribia sakaratul mauti. Alikaa kando ya mwanafunzi na kuanza kusoma Sūrah Yāsīn lakini mwanafunzi akasema, “Acha kusoma Sūrah Yāsīn.” Sayyidunā Fuḍayl bin ‘Iyād رضي الله تعالى عنه halafu akasoma Talqīn¹ (yaani kumkumbusha) kusoma Kalimah lakini akajibu, “Katu sitasoma Kalimah na hainihusu kabisa.” Aliposema maneno haya tu akafa. Sayyidunā Fuḍayl bin ‘Iyād رضي الله تعالى عنه alilia kwa siku 40 nyumbani kwake kwa ajili ya kuhuzunishwa na mwisho mbaya wa mwanafunzi huyu. Baada ya siku ya 40, alimuona mwanafunzi yule akiburutwa motoni na malaika katika ndoto. Akauliza, “Kwa nini ulinyimwa maarifa ya Mwenyezimungu عز وجل? Ulikuwa na daraja kubwa mno miongoni mwa wanafunzi wangu.” Mwanafunzi akajibu, “Ilikuwa ni kwa sababu ya tabia tatu mbaya. Ya kwanza ni kufitinisha watu, nilikuwa nikisema hivi kwa rafiki zangu na vingine kwako wewe. Ya pili ni wivu-Niliwaonea wivu rafiki zangu na ya tatu ni ulevi. Kutokana na ushauri wa daktari nilikuwa nikinywa glasi moja ya tembo kwa mwaka mara moja ili iniponeshe maradhi.” (*Minhāj-ul-‘Ābidīn, uk.165*)

Ndugu wapenzi waislamu! Tetema kwa hofu ya Allah عز وجل na umsujudie kwa unyenyekevu ili umridhishe. Lahaula! Mwanafunzi

¹ Usimwambie anayekata roho kusoma Kalimah. Badala yake isome Kalimah ukiwa karibu naye kwa sauti ili akumbuke kuisoma. Tazama namna ya kusoma Talqīn katika kijitabu ‘40 Madani Wills.’

wa mwanachuoni mkubwa alitamka Kufuru katika sakaratul mauti kwa ajili ya kufitinisha watu, wivu, na kunywa pombe. Sadr-ush-Sharī'ah, Badr-ut-Tarīqah, 'Allāmah Mufti Muhammad Amjad 'Alī A'zamī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْعَلِيِّ ameleeza, “Allah عَزَّوَجَلَّ atulinde, ikiwa mtu atatamka maneno ya Kufuru wakati anapokufa, hukumu ya kufuru haitajuzu kwake kwa kuwa inawezekana awe amepoteza busara yake kwa ajili ya mateso ya kifo, hivyo basi akasema maneno hayo bila kujua.” (*Bahār-e-Sharī'at*, juzuu ya 4, *Maktaba-tul-Madīnah, Karachi*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Kufufuliwa kwa sura ya mbwa

Inasikitisha kuwa kufitinisha watu imekuwa ni jambo la kawaida hata watu wengine pengine hawaelewi kuwa ni tendo oву. Kufitinisha watu hugaribu ahera ya mtu. Rasūlullāh صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, “Wale ambao husenganya, huwasuta wengine, hufitinisha na huwatia hatiani watu wasio na hatia; watafufuliwa (siku ya kiyama) na Allah عَزَّوَجَلَّ kwa sura ya mbwa.” (*At-targhīb Wattarhīb*, juzuu ya 3, uk.325, *Dār-ul-Kutub-ul-'Ilmiyyah, Beirut*) Imetajwa katika hadithi nyingine kuwa mtu ambaye hufitinisha watu, hataingia peponi. (*Ṣaḥīḥ Bukhārī*, juzuu ya. 4, uk. 115, *Ḥadīṣ 6056*, *Dār-ul-Kutub-ul-'Ilmiyyah, Beirut*)

Maana 'yakufitinisha watu'

Ni muhimu sana kuepuka Muḥlikāt, yaani dhambi zinazokuelekeza katika maangamizi. Ili mtu aweze kuziepuka ni

muhimu kujifunza na kuzielewa. Huu hapa ni ufafanuzi wa kufitinisha watu: ‘Allāmah ‘Aīnī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوِيّ ameeleza kutoka Imām Nawavī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْقَوِيّ, “Kumfikishia mtu maneno ya mtu mwingine kwa lengo la kuleta madhara ni kufitinisha.” (*Umda-tul-Qārī, Ḥadīṣ 216, juzuu ya 2, uk.594, Dar-ul-Fikr, Beirut*)

Je, tunajiepusha na kufitinisha watu?

Ni jambo la kusikitisha kwamba mazungumzo mengi siku hizi ni ya kufitinisha na kusengya iwe ni katika mikusanyiko ya marafiki au watu, sherehe za harusi au matanga, mikutano, au mazungumzo ya mtu kwa simu. Mtu mmakinifu akichanganua mazungumzo hayo, pengine atatambua mengi ni ya kufitinisha na ya madhambi.

Lahaula! Itakuwa vipi hali yetu? Soma hadithi hii tena. “Anayefitinisha watu hatoingia peponi”. Tutajizua kuzungumza ovyo ikiwa tu tutaweka Qufl-e-Madani¹ kwa ulimi wetu. Kawaida ni vigumu kwa wale ambao wako na marafiki waovu na wazungumzaji kujizua kufitinisha na kusengya. Hadithi nyingine inasema, “Anayesema sana hufanya makosa mengi na anayefanya makosa mengi hufanya dhambi nyingi na yule afanyaye dhambi nyingi anafaa zaidi kuingia motoni.” (*Hilya-tul-Auliya, juzuu ya 3, uk.87-88, Ḥadīṣ 3278, Dār-ul-Kutub-ul-‘Ilmiyyah, Beirut*)

¹ ‘Qufle Madina’ katika mazingira ya Madani ya Dawat-e-Islami ina maana kujizua na kuzungumza ovyo ovyo.

Mtume kipenzi na mwenye Baraka صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, “Bishara njema ni kwa mtu ambaye anajizuia kutokana na mazungumzo yasiyo na maana na hutumia kilicho cha ziada katika mali yake (katika njia ya Mwenyezimungu).” (*Al-Mu'jam-ul-Kabīr, juzuu 5, uk.71-72, Dār Iḥyā-ut-Turāṣ-ul-'Arabī, Beirut*) Swahaba mmoja رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ amesema, “Wakati mwengine mtu hunisemesha kitu nami huwa na hamu ya kumjibu zaidi kuliko hamu ya mtu mwenye kiu kwa maji ya baridi lakini hujizuia nikihofia kuwa yasiwe ni maneno ya upuuzi.” (*Ittiḥāfussāda-til-Muttaqīn, juzuu 9, uk.159, Dār-ul-Kutub-ul-'Ilmiyyah, Beirut*)

Ndugu waislamu wapenzi! Swahaba huyo رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ alijiepusha na mazungumzo yanayofaa akihofia kuwa yasiwe ni ya upuuzi ilihali sisi tukimueleza mtu jambo hatuachi kusengenya, kufitinisha, kutoa aibu za wengine, na kuwasingizia. Ah! Tutakuwaje? Allah عَزَّوَجَلَّ atupe fahamu na tawfiki ya kuweka Qufl-e-Madīnā kikweli kweli.

آمِينَ بِجَاهِ النَّبِيِّ الْأَمِينِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Ndugu wapenzi waislamu! Hadithi hiyo imeeleza pia ukorofi wa wivu. Inasikitisha kuwa maradhi ya wivu yameenea. Imeelezwa katika hadithi, “Wivu huteketeza matendo mazuri namna moto unavyoteketeza mbao.” (*Sunan Ibn-e-Mājah, juzuu 4, uk. 473, Ḥadīṣ 4210, Dār-ul-Ma'rifaḥ, Beirut*)

Maana ya wivu

Mwenye wivu anaitwa ‘Hāsīd’, ilihali yule anyeonewa wivu anaitwa ‘Maḥsūd.’ Kwa mujibu wa Lisān-ul-Arab, juzuu 3, uk. 166, maelezo ya Hasad ni;

أَلْحَسَدُ أَنْ تَتَمَنَّى زَوَالَ نِعْمَةِ الْمَحْسُودِ إِلَيْكَ

**Hasad (Wivu) ni kutamani
neema ya mwenzako iondoke kwake ije kwako.**

Maelezo mepesi ya wivu

Ndugu wapenzi waislamu! Ikiwa mtu atatamani neema ya mwenzake iondoke ije kwake, huu ni wivu. Kwa mfano, ikiwa mtu atatamani, kwa sababu ya chuki, mtu fulani maarufu au anayeheshimika aabike na badala yake yeye ndiye awe maarufu au mtu kutamani tajiri fulani awe maskini ili yeye awe tajiri.

Allah عَزَّوَجَلَّ atulinde, ugonjwa huu umeenea sana. Siku hizi watu hufanya hila za kuharibia wengine biashara zao. Hulaumiana na kutafutiana makosa ya bidhaa za wenzao. Kwa kusukumwa na wivu hudanganya, husengenya, hutoa aibu za wengine, hufedhehesha na madhambi mengine mengi. Ah! Udugu wa kiislamu umeanza kupotea kwa waislamu wengi siku hizi. Tazama namna gani waislamu wa zamani walivyokuwa wakweli kwa kusoma kisa kifuatacho:

Kisa cha Quṭb-e-Madīnah

Khalifa wa A'lā Ḥaḍrat, Quṭb-e-Madīnah, Sayyīdunā Ziyāuddīn Aḥmad Qādirī Razavī رَحْمَةُ اللهِ الْقَوِيّ alihamia Madīnah tangu wakati wa 'kipindi cha serekali ya Waturuki'. Yeye رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alikaa katika jiji lililobarikiwa takriban kwa miaka 77 na kaburi lake liko Jannat-ul-Baqī'. Siku moja mtu alimuuliza Quṭb-e-Madīnah رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ, “Yā Sayyidī! Watu wa Madina walikuwaje nyakati hizo?” (alikusudia wakati wa Waturuki) Yeye رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ akajibu, “Siku moja Al Ḥāji mmoja tajiri alikwenda duka la vitambara kununua kitambara aina fulani kwa kiasi kikubwa ili awagawanyie maskini. Mwenye duka akamwambia, “Ninacho kitambara hicho kwa kiwango unachokitaka lakini nakuomba ununue kwa duka lile linalonielekea. اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ, leo nimeuza vizuri lakini mwenzangu mwenye duka lile ameuza kidogo mno.” Sayyidī Quṭb-e-Madīnah, رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ halafu akasema, “Watu wa Madīnah zamani walikuwa wakiishi hivyo.” Allah عَزَّوَجَلَّ awarehemu na atusamehe kwa baraka yao.

Kuangamia kwa muadhini wawili waliokuwa wakipenda amrad (wavulana wazuri wanaovutia)

Sayyīdunā ‘Abdullāh bin Ahmad Mūazzin رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alisema, “Nilikuwa natufu Ka’bah nilipomuona mtu mmoja aliyekuwa ameshikilia tandiko la Ka’aba huku akiirudia Dua hii, “Ewe Allah عَزَّوَجَلَّ! Nijaalie niondoke katika ulimwengu huu ilhali mimi ni muislamu.” Nikamuuliza, “Kwa nini huombi Du’a nyingine mbali na hii?” Akajibu, “Nilikuwa na kaka wawili.

Kakangu mkubwa alikuwa akiadhini msikitini bila malipo kwa miaka 40. Wakati wa kifo chake aliomba aletewe Qur'an takatifu na tukampa ili apate baraka kutokana kwayo. Huku akiwa ameishika Qur'an mkononi, alisema, "Nyote kuweni mashahidi kwamba nakanusha maamrisha na itikadi ya Qur'an na nakubali ukristo." Aliposema hayo tu, akafa. Ndugu yangu mwengine pia aliadhini kwa miaka 30 bila malipo lakini pia alikufa akiwa si muislamu. Kwa hivyo nina wasiwasi mno na mwisho wangu na naomba mwisho mwema." Sayyidunā 'Abdullāh bin Aḥmad Mūazzin رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ akauliza, "Kaka zako walikuwa wakifanya dhambi gani?" Mtu huyo akajibu, "Walikuwa wakipenda kufanya uhusiano usio wa halali na wanawake na kuwatamani Amrad (wawulana wazuri wanaovutia)." (*Roūd-ul-Fāiq, uk.17, Dār-ul-Kutub-ul-ʿIlmiyyah, Beirut*)

Hukumu ya stara

Ndugu wapenzi waislamu! Ni msiba ulioje! Je, hatutaacha kutojisitiri na kudhihakiana na ajnabiya (wanawake ambao tunafaa kuwaoa)? Je, hatutaacha kuzuia macho yetu kutazama ajnabiya wakiwemo shemegi zetu, wake wa ami na wajomba zetu? (Kulingana na Shari'ah, hawa pia ni wanawake ajnabiya).

Vile vile binamu, mashemegi wa kike na wa kiume wanafaa kuwekeana stara. Shehe na wafuasi wake wa kike wanafaa kuwekeana stara. Mfuasi wa kike hafai kubusu mkono wa shehe wake.

Kumuangalia amrad kwa matamano ni haramu

Tahadhari! Amrad ni kama moto. Kuwa karibu naye, kufanya urafiki naye, kudhihakiana, kumshika, kumpiga pambaja ni matendo yanayoweza kumtia mtu motoni. Ingawa maskini hana makosa, kuna usalama ukijiepusha naye. Wala usimfanye ahisi kwamba anaonewa kwa kuwa yeye ni Amrad.

Hata hivyo ni muhimu kwako wewe kumuepuka. Usikae nyuma yake wala asikae nyuma yako katika pikipiki kwani huenda matamano yakawafikia. Hata ikiwa hakuna matamano, kumkumbatia kunaweza kusababisha fitna. Ikiwa mtu ana matamano, basi kumkumbatia, kupeana mikono, na kwa mujibu wa baadhi ya wanachuoni, hata kumuangalia kwa matamano ni haramu. (*Tafsīr-e-Aḥmadīyyah*, uk.559, Peshawar)

Yahifadhi macho yako kuangalia sehemu yoyote ya mwili wake na hata nguo zake. Ikiwa mtu anahisi matamano kwa kumfikiria basi hili liepukwe pia. Vile vile, ikiwa mtu atahisi matamano kwa kuangalia muandiko wake, nyumba yake, babake, kakake au yeyote au chochote kilicho chake, basi mtu ajizue kumtazama mtu huyo na kitu hicho.

Amrad ana mashetani sabini

A'lā Ḥaḍrat رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ katika kututahadhrisha kuhusu namna shetani anavyotushambulia kupitia Amrad amesema, “Inasemekana kuwa mwanamke ana mashetani wawili ilihali Amrad ana mashetani sabini.” (*Fatāwā-e-Razavīyyah*, juzuu.23, uk.721) Hata hivyo

ni muhimu kujitenga na kujizuia kuwaona Amrad na mwanamke ajnabiya. Umeona namna gani kaka wawili walioonekana kuwa wacha Mungu walivyokikabili kifo chao.

Tafadhali kipitie kijitabu cha Maktaba-tul-Madīnah, ‘Amrad Pasandī kī Tabāḥkāriyān’.

*Nafs bay lagām to gunāḥaun pay uksātā ḥay
Taubāḥ taubāḥ karnay kī bhī ‘ādat ḥonī chāhiye*

Kutohiji ni sababu ya mwisho mbaya

Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ametoa tahadhari, “Mtu ambaye ana uwezo wa kuhiji na hana dharura iliyowazi, kiongozi mgandamizaji wala ugonjwa; akifa bila kwenda hajj basi afe aidha kama myahudi au naswara.” (*Sunan Dārimī, juzuu.2, uk. 45, Hadīṣ 1785, Bāb-ul-Madīnah, Karachi*)

Hii inaonyesha kuwa yule aliyekufa bila kwenda hajj ilhali imemlazimu, yuko katika hatari kubwa ya kuishia na mwisho mbaya.

Hofu ya mwisho mbaya kwa anayezungumza wakati wa adhan

Akirejelea Fatāwā-e-Razavīyyah, Sadr-ush-Sharī’ah, Badr-ut-Tarīqah, “Allāmah Muftī Muhammad Amjad ‘Ali A’zamī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللهِ الْقَوِي amesema, “Yeyote anayeendelea kuzungumza wakati muadhini anaadhini yuko hatarini ya kufikwa na

Sababu za Mwisho Mbaya

mwisho mbaya. Allah ﷺ atuepushe.” (*Bahār-e-Sharīʿat*, juz. 3, uk. 41, *Maktaba-tul-Madīnah, Karachi*)

Aliyefuatiliza adhana aingia peponi

Ndugu waislamu wapenzi! Adhana inapoanza, mtu asimamishe kile anachokifanya na aifuatilizie. Ikiwa, mtu anatembea kuelekea Masjid au anatawadha, anaweza kuendelea huku akiifuatilia. Ikiwa kuna adhana nyingi zinaadhiniwa, inatosheleza kufuatilia ya kwanza peke yake. Hata hivyo ni bora kuzifuatilia zote.

Waliobahatika kweli ni wale wanaofuatilia adhana! Imeelezwa katika *Tārīkh-e-Dimishq*, juzuu ya 40, uk. 412, ‘Sayyīdunā Abū Hurairah رضي الله تعالى عنه amesema kwamba mtu mmoja ambaye alikuwa hajulikani kwa matendo yake mema alikufa. Mtume Mtukufu صلى الله تعالى عليه وآله وسلم akawaambia maswahaba wake رضي الله تعالى عنهم, “Je, mwajua kuwa Allah ﷺ amemuingiza mtu yule peponi?” Maswahaba رضي الله تعالى عنهم wakashangazwa na hili kwa sababu hakufanya amali yoyote yakuonekana. Baadaye, swahaba wake mmoja رضي الله تعالى عنه alikwenda kwa nyumba ya marehemu na akamuuliza mkewe kuhusu amali yoyote njema aliyokuwa akifanya mumewe. Akajibu, “Sijui amali yoyote mahususi lakini ninachojua ni kwamba alikuwa akiifuatilia adhana kila alipoisikia ikiwa ni mchana au usiku.” (*Tārīkh-e-Dimishq cha Ibn ‘Asākir*, juz40, uk412, *Dār-ul-Fikr, Beirut*)

Allah ﷺ awarehemu na atusamehe kwa baraka yao!

Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu hukumu ya adhana na kuifuatilia pitia kitabu cha Maktaba-tul-Madīnah, ‘Faizān-e-Azān.’

Mlima wa moto

Sayyīdunā Mālik bin Dīnār عليه رَحْمَةُ اللهِ الْعَظِيمَا siku moja alikwenda kumtembelea mtu ambaye alikuwa akaribia kufa. Yeye رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alimuhimiza mara kwa mara kupiga shahada lakini (Yule mtu) aliendelea kusema, “Kumi, kumi na moja! Kumi, kumi na moja!” Mtu Yule alipoulizwa sababu ya kusema vile, alijibu, “Kuna mlima wa moto mbele yangu; kila ninapojaribu kupiga shahada mlima unanikaribia ili unichome.” Yeye رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ akawauliza watu kuhusu amali aliyokuwa akiifanya mtu yule katika uhai wake. Watu wakamjibu kuwa alikuwa mla riba na akiibia watu katika mizani (alipokuwa akiwapimia bidhaa kuwauzia). (*Taḥkirah-tul-Auliya, uk 52-53, Tehran*)

Adhabu ya udanganyifu katika mizani

Ole wao! Maangamizi yawangojea wale wanaokula riba na kufanya udanganyifu katika mizani. Enyi munaojijasirisha kujirusha katika miali ya moto kwa ajili ya vijisenti kidogo! Sikilizeni! Imeelezwa katika Rūḥ-ul-Bayān, “Anayedhulumu katika mizani atarushwa katika kina cha moto siku ya Qiyama na atawekwa katikati ya milima miwili ya moto, halafu ataamrisha kuipima. Akiikaribia milima, moto utamchoma.” (*Rūḥ-ul-Bayān, juz 10, uk 364, Quetta*)

Mwisho mbaya wa shehe

Inasimuliwa kwamba Sayyidunā Sufyān Šaurī na Sayyidunā Shaybān Rā’ī رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى walikutana. Sayyidunā Sufyān Šaurī رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى akaendelea kulia usiku kucha. Sayyidunā Shaybān Rā’ī رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى alipomuuliza sababu ya kufanya hivyo, alijibu, “Nalia kwa kuhofia mwisho mbaya wakati wa kifo changu. Nilipata mafunzo ya dini miaka 40 kutoka kwa shehe mmoja. Shehe huyu alifanya ibada kwa miaka 60 katika Masjid-ul-Ḥarām lakini akafa katika ukafiri. Sayyidunā Shaybān Rā’ī رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى akasema, “Ewe Sufyān! Haya ni matokeo ya dhambi zake: Usimuasi Allah عَزَّوَجَلَّ hata kidogo.” (*Sab’a Sanābil, uk 34, Maktaba Nūrīah Razavīyyah, Sakhar*)

Mwalimu wa zamani wa malaika

Ndugu Waislamu! Allah عَزَّوَجَلَّ hamtegemei mtu yeyote. Hakuna anayejua mipango yake. Mtu yeyote asijiringie elimu au ibada yake. Iblis alifanya ibada kwa maelfu ya miaka mpaka akawa ‘Mwalimu wa Malaika’. Lakini aliangamizwa kwa kuwa na kiburi na akakosa imani. Sasa hutumia nguvu zake zote kupotosha watu katika uhai wao kwa kuwanong’onezea manong’ono ya kuwapoteza na mtu anapokaribia kufa, Iblis hutumia uwezo wake wote kumpotosha imani yake.

Shetani katika sura ya wazazi

Mtu anapokaribia kufa, shetani wawili huja kumkalia mkono wa kulia na kushoto kwa sura za wazazi wake (yule anayekufa),

shetani wa mkono wa kulia husema, “Ewe mwanangu! Tazama, mimi ni babako mpole na mwangalizi. Nakushauri usife ila baada ya kuingia katika Ukristo kwani ni dini bora kuliko zote.” Shetani wa mkono wa kushoto (katika sura za mama) husema, “Ewe mwanangu kipenzi! Nimekuweka tumboni mwangu. Nimekunyonyesha maziwa yangu na kukuongoa mapajani mwangu. Ewe mwanangu! Nakushauri usife ila baada ya kuukubali Uyahudi kwani ni dini bora kuliko zote.” (*Taḏkirah̄ cha Imām Qurṭubī, uk 38, Dār-ul-Kutub-ul-‘Ilmiyyah, Beirut*)

Tone la maumivu ya kifo

Ndugu waislamu! Hakika hii ni hali ya kushtua. Mtu anapokuwa na homa au kuumwa na kichwa hupata shida kufanya uamuzi wa sawa. Maumivu ya kifo ni makali mno. Imeelezwa katika Sharḥ-us-Ṣudūr kwamba ikiwa tone moja la maumivu ya kifo litaangushwa kwa wale (viumbe) wote wanaoishi angani na ardhini, basi wote watakufa. (*Sharḥ-us-Ṣudūr, uk32, Dār-ul-Kutub-ul-‘Ilmiyyah, Beirut*) Ni hali ngumu iliyoje kuwa imara katika uislamu ikiwa shetani atamjia aliye katika sakaratul mauti kwa umbo la wazazi wake ili amghilibu katika wakati mgumu kama huo. Katika Kimīyā-e-Sa’adat, ‘Sayyidunā Abū Dardāḥ رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ amesema, “Naapa kwa jina la Allah عَزَّوَجَلَّ ya kwamba hakuna mwenye hakika iwapo atakufa katika Uislamu au la.” (*Kimīyā-e-Sa’adat, juz 2, uk 825, Tehran*)

Shetani kwa sura za marafiki

Hujja-tul-Islam Sayyīdunā Imām Muhammad Ghazālī عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللَّهِ الْوَالِيّ amesema, “Wakati wa sakaratul mauti, shetani na washiriki wake humjia yule anayekata roho kwa sura za rafikize na jamaa zake. Wanamwambia, “Ndugu! Tumeonja mauti kabla yako. Sote tunajua kinachofanyika baada ya kifo. Sasa ni wakati wako. Tunakupa ushauri ujiunge na Uyahudi kwa sababu ni dini ya pekee ambayo anaikubali Allah ﷺ.” Ikiwa anayekata roho atakataa wanayoyasema mashetani hawa, wanajitokeza kwa sura za marafiki zake wengine na kumshauri, “Kubali Ukristo kwani ni dini iliyobatilisha dini ya Musa.” Kwa njia hii makundi mbali mbali ya mashetani humjia kwa sura za marafiki na jamaa zake na kumshawishi ajiunge na madhehebu yasiyo ya kweli (na imani). Hivyo basi, yule aliyejaaliwa kuupa mgongo ukweli (Uislamu) hubabaika na hukubali batili (dini isiyo ya kweli).” (*Dur-rah-tul-fākhirah, Dār-ul-Kutub-ul-‘Ilmiyyah, Beirut*)

Tutakuwaje?

Allah ﷺ awe na rehema juu yetu. Hatujui itakuaje wakati wa kifo chetu. Tumefanya dhambi nyingi na hatuna amali njema. Ewe Allah ﷺ! Tunakuomba umzuie shetani kutujia wakati wa kifo na utujaalie kumuona Mtume wako kipenzi صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ.

Udhibiti ulimi wako

Ndugu waislamu wapendwa! Kila muislamu daima aogope mipango ya siri ya Allah ﷺ. Haijulikani ni matendo gani

maovu ambayo yanaweza kusababisha ghadhabu ya Allah ﷺ na kuhatarisha imani. Daima uwe mnyenyekevu kwa Allah ﷺ. Udhibiti ulimi wako kwani kuropoka wakati mwengine husababisha mtu kutamka maneno ya kufuru bila ya kujua. Ni wajibu daima mtu kujishughulisha kuhifadhi imani. A'lā Ḥaḍrat ṛḥمته اللہ تعالیٰ علیہ ameeleza kwamba wanavyuoni wamesema, “Ambaye hana hofu ya kupoteza imani yake (katika maisha yake) yuko hatarini kuipoteza (imani yake) wakati wa mauti yake.” (*Malfūz Sharīf, V4, P390, Hāmid & Company, Lahore*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Maua ya madanī kwa mwisho mwema

Ndugu wapenzi waislamu! Ni jambo la kutia hofu sana kwa kuwa hatujui Allah ﷺ ametupangia nini. Hatujui mwisho wetu utakuwaje. Ḥujja-tul-Islam Sayyidunā Imām Muhammad Ghazālī ṛḥمته اللہ الوالی amesema, “Ikiwa unataka kuwa salama kutokana na mwisho mbaya, tumia uhai wako wote kumtii Allah ﷺ na uepuke dhambi ya aina yoyote. Ni muhimu kuwa na hofu kama ya ‘Aārīfīn (mawalii) ili ulie sana na uwe na huzuni wakati wote. Yeye ṛḥمته اللہ تعالیٰ علیہ ameeleza zaidi, “Daima fanya bidii kupata mwisho mwema. Daima jishughulishie kufanya dhikri ya Allah ﷺ. Ondosha mapenzi ya ulimwengu moyoni mwako. Vikinge viungo na moyo wako na dhambi. Jiepushe hata kuwatazama watu waovu kwa sababu moyo huathirika kwayo na akili yako huenda ikaelekea upande wao.” (*Ihyā-ul-‘Ulūm, juz4, uk219, Beirut*)

Maombi manne ya kifo chenye imani

Mtu mmoja alikuja kwa A'lā Ḥaḍra رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ na akamuomba amuombe dua ili apate kifo kizuri chenye imani. A'lā Ḥaḍrat رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ akamuomba dua na akampa ushauri ufuatao:

1. Soma يَا حَيُّ يَا قَيُّوْمُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ mara 41 kila siku asubuhi na umswalie Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ mara moja kabla na baada yake.
2. Soma sura Kāfirūn unapokwenda kulala baada ya kuomba maombi mengine yote. Halafu nenda kulala bila kuzungumza na mtu yeyote. Hata hivyo unaweza kuongea inapobidi lakini usome sura Kāfirūn tena. إِنَّهَا أَلَمَ اللَّهُ مَعَرَّوَجَلٌ, utakufa katika imani.
3. Soma اللَّهُمَّ إِنَّا نَعُوذُ بِكَ مِنْ أَنْ نُشْرِكَ بِكَ شَيْئًا نَعْلَمُهُ وَنَسْتَغْفِرُكَ لِمَا لَا نَعْلَمُهُ asubuhi na jioni mara tatu tatu. (*Malfūz Sharīf, juz 2. uk 234, Ḥāmid & company, Lahore*)
4. Soma بِسْمِ اللَّهِ عَلَى دِينِي بِسْمِ اللَّهِ عَلَى نَفْسِي وَوُلْدِي وَأَهْلِي وَمَالِي¹ asubuhi na jioni mara tatu tatu, utapata ulinzi wa dini yako, imani, uhai, mali na familia. (*Shajarah-e-Qādiriyah Razavīyah, Maktaba-tul-Madīnah, Karachi*)

(Usiku ni kuanzia kuzama jua hadi kupambauka. Asubuhi ni kuanzia usiku wa manane hadi kuchomoza jua.)

¹ Tafsiri: Ewe Allah ﷻ! Tunajilinda kwako kutokana na kukushirikisha wewe na kitu chochote kwa kujua na tunaomba msamaha kwa kukushirikisha kwa kutojua.

² Tafsiri: Kwa wema wa jina la Allah ﷻ, imani, maisha, watoto, familia na mali ilindwe!

Masanduku ya moto

Ndugu wapenzi waislamu! Mtu mwenye bahati mbaya ni yule anayekufa katika hali ya kukufuru. Atabanwa na kaburi kwa nguvu mno mpaka mbavu zake za kulia zitapishana na za kushoto. Kutakuwa na adhabu nyengine nyingi kali sana kwa makafiri. Watakaa miaka 50,000 ya siku ya hukumu katika hali ya kutisha mno. Halafu wataburutwa kwa uso watupwe motoni.

Waislamu waliotenda dhambi, ambao wameingia motoni, watatolewa na kuwaacha wale tu waliokufa katika kufuru. Mwishowe kila kafiri atafungiwa katika sanduku la moto linalomtosha kuingiza mwili. Litajazwa moto. Halafu kufuli ya moto itawekwa katika sanduku hili. Sanduku hili halafu litawekwa ndani ya sanduku lingine. Katikati ya masanduku haya kutawashwa moto. Kufuli la moto litawekwa tena katika sanduku hili. Sanduku hili baadaye litawekwa tena ndani ya sanduku moja zaidi la moto lenye kufuli la moto. Halafu kifo kitaletwa kwa umbile la kondoo na kuchinjwa katikati ya peponi na motoni. Kuanzia hapo hakuna atakayekufa tena. Kila aliye peponi ataishi milele peponi na kila aliye motoni ataishi milele motoni. Watu wa peponi watazidi kuwa na furaha na watu wa motoni watazidi kuwa na majuto. (*Bahār-e-Sharī'at, juz 1, uk 88, 91-92, Maktaba-tul-Madīnah, Karachi*)

Ewe Allah **عَزَّوَجَلَّ**! Tunakuomba utujaalie kifo cha amani na imani, tufe mashahidi katika mji mtakatifu wa Madīnah, tuzikwe Jannat-ul-Baqī' na tupate kuwa jirani wa Mtume wako Mtukufu **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** katika Jannat-ul-Firdaus.

Ndugu waislamu wapendwa! Musikate tamaa kuipata huruma ya Allah ﷺ. Ukifanya desturi ya kusafiri na Madanī Qāfilāh ya Dawat-e-Islami, utakuza fikra ya kulinda imani yako ﷺ. Na ukisha kuwa na fikra ya kulinda imani yako basi utakuwa na msimamo na utazidi kumuomba Allah ﷺ kwa unyenyekevu.

Kulia kwa mtume Mtukufu ﷺ

Weka mkono juu ya moyo na usikilize namna gani Mtume wetu kipenzi aliyebarikiwa ﷺ alivyokuwa na wasiwasi juu ya usalama wa imani yetu. Imeelezwa katika juzuu ya 10 Rūḥ-ul-Bayān ukurasa wa 315 kwamba siku moja shetani akiwa amejibadilisha sura alikuja kwa Mtume Mtukufu ﷺ akiwa na chupa ya maji mkononi na akasema, “Nina wauzia watu chupa hii wakati wa kifo chao kwa kubadilishana na imani yao.” Kusikia hayo, Mtume Mtukufu ﷺ akalia sana mpaka watu wa familia yake nao pia wakaanza kulia. Allah ﷺ akatuma wahyi, “Ewe kipenzi changu! Usiwe na huzuni. Nawalinda waja wangu wakati wa kifo chao kutokana na udanganyifu wa shetani.” (*Rūḥ-ul-Bayān, juz.10, uk.315, Quetta*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Baraka Za Sunnah

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِي كَاتَبَنَا بِالسُّنَنِ الْكَامِلَةِ وَالْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِي كَاتَبَنَا بِالسُّنَنِ الْكَامِلَةِ
Katika mazingira ya Dawat-e-Islami (shirika la harakati ya Quran na Sunnah la kimataifa lisilo jihusisha na siasa) tuna funza na kufundisha Sunnah za Bwana Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Hudhuria ijtimai ya kila wiki siku ya al-khamis baada ya sala ya magrib inayofanyika katika mji wako. Safiri pamoja na wapenzi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ katika Madani Qafilah na uweke azma yakujaza kadi ya zawadi 72 za Madina (Madani In'amaat) na kumkabidhi msimamizi (Zimmedaar) kila mwezi. Kwa Baraka ya kufanya hivi اِنْ شَاءَ اللهُ tutzaweza kushikamana na Sunnah za Bwana Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na tutachukia maasi na tutaweza kulinda imani yetu.

Kila moja aweke azma hii "Ninataka kusuluhisha nafsi yangu na watu wa ulimwengu mzima اِنْ شَاءَ اللهُ عَزَّوَجَلَّ". Kusuluhisha nafsi yangu nita fuata "Madani In'amaat" na kusuluhisha nafsi za watu wa ulimwengu mzima nita safiri katika "Madani Qafilah" اِنْ شَاءَ اللهُ عَزَّوَجَلَّ.

